

9B-Lahnul-khafiy: (Makosa [Madogo] Ya Kufichika)

2- لحن الخفي - Lahnul-khafiy (Makosa [Madogo] Ya Kufichika)

Makosa haya kama jina linavyoashiria ni yale yote yaliyojificha, nayo ni yale makosa yakiufundi; ufundu wa kuisoma Qur-aan kwa kutumia fani hii ya Tajwiyd; kwa kweli ni makosa ambayo hayawezi kuelewaka na kugundulika isipokuwa kwa wale wenye kuilewa fani ya Tajwiyd pekee, kwani si kila msomaji wa Qur-aan huweza kuyahisi na kuyagunduwa kwa kuwa yamejificha hayako wazi. Pia ni vyema ieleweka kuwa makosa haya hayaharibu wala hayabadilishi wala hayapotoshi maana iliyotakiwa kuthibitishwa iwe ni neno au Aayah nzima, kwani yanahusiana zaidi na utowaji wa sauti kulingana na pahala ilipo herufi fulani, au utowaji wa sauti kulingana na alama ya *i'raab* iliyo juu ya herufi fulani na kadhalika. Hukmu yake makosa haya ni *makruwh* (yanachukiza).

Mfano: Kutotamka herufi zipasazo kwa *tafkhiym* (mdomo kujaa) kama vile herufi ya, inapokuwa na *i'raab* ya fat-hah au imetanguliwa na herufi yeny*e i'raab* isiyokuwa kasrah hutakiwa itamkwe kwa *tafkhiym*. Makosa mengine ni kukosa kuchunga na kufuata hukmu za *ghunnah*, *ikhfaa*, *idghaam* na baadhi ya *madd*. Na kwa hakika yanachukiza kwani yanainyima Qur-aan utamu wake; hivyo inampasa mwenye kuisoma Qur-aan kujiepusha nayo kwa kujifunza fani ya Tajwiyd .